**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA SABA

**03 FEBRUARI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 03 FEBRUARI, 2016

## I. MASWALI:

### OFISI WAZIRI MKUU:

**77. MHESHIMIWA JOHN WEGESA HECHE (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wakati wa Kampeni za Urais mwaka 2015 Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliwaahidi Wananchi wa Mji wa Nyamwaga kuwa ataanzisha mchakato wa kuwalipa wazee pensheni zao kwa wakati:-

Je, mpango huo muhimu utatekelezwa lini.

### OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**78. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Kumekuwepo na malalamiko mengi ya Walimu kulipwa mishahara midogo ambayo hailingani na gharama halisi za maisha:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha maslahi ya walimu.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**79. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kata za Semembela, Isagenhe na Kahama ya Nhalanga hazina kabisa Mawasiliano ya Simu za Mkononi:-

Je, ni lini Kata hizo zitapatiwa huduma hiyo muhimu ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi.

**80. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Bodi ya barabara ya Mkoa wa Rukwa ilishaomba kwamba barabara za Kitosi – Wampembe na Nkana – Kala kuchukuliwa na Mkoa; na Serikali imeendelea kuzifanyia matengenezo ya dharura ili zipitike kilio cha barabara hizo kilifikishwa kwa Rais pamoja na Makamu wa Rais wa awamu ya tano na wote walitoa ahadi ya kuziboresha barabara hizo:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuzipandisha hadhi barabara hizo;

(b) Je, ni lini Serikali itaitikia kilio hicho cha Wananchi wanaopata shida kwa barabara hizo kutopitika katika kipindi chote cha mwaka.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**81. MHESHIMIWA OSCA RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio ya ujambazi unaohusiana na uporaji wa fedha; na ni muhimu sana Watanzania wakapata ufahamu kwa takwimu kuhusu ukubwa au udogo wa tatizo hilo kuliko kupata taarifa ya tukio moja moja:-

(a) Je, ni zipi takwimu sahihi na mchanganuo wa matukio ya ujambazi unaohusiana na uporaji wa fedha ikiwa ni pamoja na vifo na majeruhi wa matukio hayo kuanzia mwaka 2013 hadi 2015 kitaifa;

(b) Je, ni mikoa gani miwili inayoongoza na mikoa gani miwili yenye matukio hayo machache.

**82. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Matukio ya Wananchi kujichukulia sheria mkononi yamezidi kuongezeka siku hadi siku na kusababisha madhara na vifo kwa watu wasio na hatia:-

Je, Serikali inafanya juhudi gani ili kupunguza au kuondoa kabisa ukatili huo.

**83. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa kuwa barabara kuu kwenda Mikoani zina foleni na tukiangalia barabara hizo zinatumika na magari mengi ya mizigo ambayo mara nyingi huwa ni chanzo cha ajali na Watanzania wengi kupoteza maisha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ajali hizo zinapungua.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**84. MHESHIMIWA UPENDO FURAHA PENEZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali ya awamu ya tano imeonyesha nia ya kutaka kuongeza mapato kwa ufuatiliaji na kuondokana na ukwepaji kodi bandarini, lakini kwa miaka mingi Serikali imekuwa ikikosa mapato kwa kutoa misamaha ya kodi kwa Kampuni za uwekezaji katika sekta ya madini:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuondokana na misamaha ya kodi inayotolewa kwa kampuni za uwekezaji.

**85. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 imelenga kuanzisha mfuko mkubwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi na wajasiriamali wadogo kwa masharti nafuu:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa jambo hilo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**:

**86. MHESHIMIWA RASHID SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu; na Watanzania zaidi ya 75% wanategemea kilimo kama ajira kwa kuendesha maisha yao:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha miradi mikubwa ya kuhifadhi maji (water reserve) ili kuwa na 'scheme' itakayowezesha wakazi wa kata za Mnazi, Lunguza na Mng'aro kuendesha shughuli zao za kilimo kwa msimu mzima.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**87. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Mabaraza ya Makundi Maalum ya Kijamii kama Wanawake, Vijana, Wazee, Watoto na Walemavu ni vyombo muhimu katika kuwaunganisha kimaendeleo:-

(a) Je, ni lini Serikali itawasilisha taarifa ya tathmini ya utendaji wa mabaraza ya Watoto na Walemavu;
(b) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuwezesha kufanya kazi kwa Baraza la Vijana la Taifa baada ya sheria yake kupitishwa;

(c) Je, ni lini Serikali itawezesha kuundwa kwa baraza la Wanawake la Taifa ili kuwaunganisha katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

**88. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ugonjwa wa kipindupindu umeendelea kukatisha maisha ya watu wengi hapa nchini, japokuwa chanzo chake ni uchafu ambao ungeweza kuzuilika:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa nchini.

## WIZARA YA MALIASII NA UTALII:

**89. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasii na Utalii:- Wananchi wa bonde la Mwakaleli Kata za Kandete, Isange na Luteba wanaoishi kando ya Hifadhi ya TANAPA wamekuwa wakinyanyaswa sana na watumishi wa TANAPA kwa kisingizio kwamba wamevamia Hifadhi wakati TANAPA ndio waliovamia makazi ya Wananchi kwa kuweka mipaka mipya tofauti na ile ya zamani hali

inayofanya baadhi ya shule na taasisi zingine kuonekana kuwa ndani ya Hifadhi ya TANAPA kwa sasa:-

Je, ni lini Serikali itarudisha mipaka ya zamani ili Wananchi wasiendelee kuishi kwa wasiwasi lakini pia waendelee na shughuli za kilimo kama ilivyokuwa zamani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**90. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi:- Serikali imedhamiria kuanzisha mfumo wa utoaji wa elimu ya msingi mpaka kidato cha nne bure, jambo litakaloanzisha wahitaji wa elimu ya kidato cha tano, sita na kisha Chuo Kikuu; Mkoa wa Katavi kwa dhamira safi ulianzisha zoezi la ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo lakini kwa bahati mbaya zoezi zima la ujenzi wa chuo hicho limegubikwa na sintofahamu na suala zima kuwa na usiri na utata:-

(a) Je, ni lini ujenzi huo muhimu utaanza;

(b) Je, ni kwa nini jambo hili lisiwekwe wazi kwa Wananchi ili kuondoa sintofahamu kutokana na usiri uliopo.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

**91. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha wakulima wanapata pembejeo za kilimo kama mbolea kwa wakati kwa kuwa tatizo hilo limekuwa sugu.

## II. KAMATI YA MIPANGO:

**(Majadiliano yanaendelea)**

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **03 FEBRUARI, 2016** | **KATIBU WA BUNGE** |